

UMUHIMU WA UONGEZAJI HISA NA AKIBA

1. HISA

Hisa ni fedha inayowekwa na Mwanachama kwa ajili ya kuwa sehemu ya Wamiliki wa Chama.

Chama kinaweza kuwa na aina mbili (2) za hisa; yaani hisa ya lazima/Uanachama/msingi na Hisa ya Hiari.

Hisa ya Lazima/Uanachama/Msingi:

- Muundo: Mfn: Mafungu 10@ Tsh. 10,000 = Jumla ya Hisa Tsh. 100,000
- Humfanya Mwanachama kuwa Mmiliki wa Chama
- Mwanachama atakuwa na sifa ya kupatiwa huduma ndani ya Chama endapo imelipa 50% au zaidi
- Hairuhusiwi kutumika kama dhamana ya mkopo
- Hupata faida ya gawio
- Ni sehemu ya Mtaji wa Chama (Mtaji Tete) [Leseni, uwekezaji, taswira, kanuni]
- Ni fedha maalum kwa ajili ya uwekezaji wa Chama
- Ni dhima ya Mwanachama kuchangia endapo Chama kitakua katika hali ya kufilisiwa
- Hisa zifanyiwe tathmini kila baada ya miaka 3; Kif 46(3) SVU, 2013
- Hisa hizi zinaweza kuuzwa kwenye soko la hisa (DSE) – “kuna changamoto nyingi”

Hisa za Hiari:

- Ni kiasi chochote cha fedha kinachoongezeka juu ya hisa za Uanachama/lazima (**tafsiri ya zamani**)
- Muundo: Mfn: Mafungu 5@ Tsh. 5,000 = Jumla ya Hisa Tsh. 25,000
- Ni fedha inayowekwa na Mwanachama muda wowote na kutolewa muda wowote (*Inaweza kuwekezwa kwa muda maalum*)
- Ni muhimu hisa ya hiari kuwa na Kasma yake inayojitegemea
- Hupata faida ya Riba
- Huweza kutumika kama dhamana ya mkopo
- Ni dhima ya Chama
- Huweza kutengenezewa aina maalum ya zao la mkopo

Akiba:

- Akiba ni fedha anayowekeza Mwanachama ndani ya Chama kwa malengo binafsi ikiwemo kukopa, kukuza ukwasi na uwekezaji.
- Akiba ni mali ya Mwanachama unakoma Uanachama inarudi kwako
- Kuna shuhuda nyingi za Wanachama walionufaika na akiba zao kwenye SACCOS ikiwemo kunufaika na mikopo kwa dhamana ya akiba, kupunguza gharama ya mkopo, kupata faida juu ya akiba, kunufaika na mafunzo, uongozi pamoja na uwekezaji.
- Kwa upande wa CHAMA akiba inasaidia kuongeza nguvu fedha (ukwasi) na uwezo wa Chama kukopesha mikopo mingi ya aina mbalimbali, lakini pia kuongeza viwango vya mikopo, kupunguza masharti ya mikopo na kupunguza hatari za ukwasishaji. Aidha, hupunguza malalamiko ya Wanachama: MWANACHAMA CHAMA MWANACHAMA



2. Mikakati ya Chama kuhamasisha Akiba

- (i) Aina za Akiba (Akiba ya lazima; Akiba za Malengo Maalum kama vile Watoto, Elimu, Kustaafu kwa Ufahari, Biashara, sinking fund)
- (ii) Kiwango cha chini kwa kila aina ya akiba
- (iii) Vigezo na masharti kwa kila aina ya akiba
- (iv) Kuongeza kiwango cha chini cha akiba kila mwaka/miaka miwili

- (v) Kuhamasisha uchangiaji wa akiba zaidi ya kiwango cha chini mfo. 21,500; 27,000; 29,150; 48,300
- (vi) Wezesha akiba kupata riba na ikiwezekana riba iongezeka kila mwaka
- (vii) Wezesha riba kulipwa mara 2 au 4 kwa mwaka
- (viii) Wezesha riba kulipwa kwa mfumo wa “compounding”
- (ix) Zao la advance riba ya akiba
- (x) Weka Wanachama katika madaraja matatu (A Tsh. 20,000 – 50,000; B Tsh. 51,000 – 100,000 na C Zaidi ya Tsh. 100,000) weka mikakati ya kimasoko/kibiashara kuhamasisha kila kundi
- (xi) Fanya shughuli za uzengezi kwa kutembelea na kuhamasisha makundi B na C
- (xii) Programu za promosheni ya akiba
- (xiii) Proposal za akiba kwa Wanachama wenye uwezo mkubwa
- (xiv) Viongozi kuwa vinara wa uwekaji akiba
- (xv) Boresha mahusiano na Wadau Wakuu (Mwajili, Mrajis, Viongozi mbalimbali, n.k)
- (xvi) Program ya elimu na mafunzo kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji
- (xvii) Motisha ya uwekaji akiba
- (xviii) Matumizi ya mifumo ya TEHAMA
- (xix) Ubia Mkakati kwa Maendeleo Endelevu

KAZI KATIKA MAKUNDI:

JE KUNA UMUHIMU WA KUONGEZA AKIBA KWENYE CHAMA CHETU?

Ndiyo

Hapana

KAMA JIBU NI NDIYO, UNA SHAURI NINI KIFANYIKE KWA KILA MWANACHAMA?